**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | Kuteuliwa na Rais |
| 2. Mhe. Omar Othman Makungu | Mwanasheria Mkuu |
| 3.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 4.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 5.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 6.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | Jimbo la Magogoni |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Jimbo la Mgogoni |
| 8.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 11.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 12.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 13.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 14.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 16.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 17.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake |
| 18.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 19.Mhe. Farida Amour Moh'd | Nafasi za Wanawake |
| 20.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Kuteuliwa na Rais |
| 21.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 22.Mhe. Haji Faki Shaali | imbo la Mkanyageni |
| 23.Mhe. Haji Mwadini Makame | Jimbo la Nungwi |
| 24.Mhe. Haji Omar Kheri | Jimbo la Tumbatu |
| 25.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 26.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 27.Mhe. Haroun Ali Suleiman | Jimbo la Makunduchi |
| 28.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 29.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 30.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 31.Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Jimbo la Chwaka |
| 32.Mhe. Jaku Hashim Ayub | Jimbo la Muyuni |
| 33.Mhe. Juma Duni Haji | uteuliwa na Rais |
| 34.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 35.Mhe. Machano Othman Said | Jimbo la Chumbuni |
| 36.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |
| 37.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 38.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | Jimbo la Kiembesamaki |
| 39Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 40.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 41.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 42.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 43.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | Jimbo la Chambani |
| 44.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | Kuteuliwa na Rais |
| 45.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Jimbo la Mpendae |
| 46.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Nafasi za Wanawake |
| 47.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 45.Mhe. Mussa Khamis Silima | Jimbo la Uzini |
| 46.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 47.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 48.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | Jimbo la Dimani |
| 49.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | Jimbo la Mtoni |
| 50.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 51.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 53.Mhe. Omar Yussuf Mzee | Kuteuliwa na Rais |
| 54.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 55.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Rashid Seif Suleiman | Jimbo la Ziwani |
| 57.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 58.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 59.Mhe. Said Ali Mbarouk | Jimbo la Gando |
| 60.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 61.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 62.Mhe. Salma Moh'd Ali | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 65.Mhe. Salum Amour Mtondoo | Jimbo la Bububu |
| 67.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 68.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | imbo la Mwanakwerekwe |
| 69.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Jimbo la Dole |
| 70.Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya | Kuteuliwa na Rais |
| 71.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 72.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 73.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 74.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Jimbo la Fuoni |
| 75.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 76.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 77.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |
| 78.Mhe. Zahra Ali Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 79.Mhe. Zainab Omar Mohammed | Kuteuliwa na Rais |

**Kikao cha Tatu – Tarehe 12 Novemba, 2010**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**Mhe. Spika:** Wajumbe wanakaa kwenye viti vyao.

## UCHAGUZI WA WAJUMBE WATANO WA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUINGIA KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Mhe. Spika:** Mkurugenzi wa Uchaguzi Katibu wa Baraza kuhusu utaratibu wa upigaji kura.

**Katibu:** Waheshimiwa Wajumbe kama tulivyotoa taarifa kuanzia jana kwamba tunakwenda kwenye uchaguzi wa wajumbe watano wa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika uchaguzi huu kuna makundi manne. Kundi 'A' lina wagombea sita ambao ni wanaume kutoka CCM. Katika kundi hilo tunatakiwa tuchague wagombea wawili. Kundi 'B' lina wagombea watatu ambao ni wanaume kutoka CUF tunatakiwa tuchague mmoja. Kundi 'C' lina wagombea watatu wanawake kutoka CCM tunatakiwa tuchague mmoja. Kundi 'D' lina wagombea watatu wanawake kutoka CUF tunatakiwa tuchague mmoja. Lakini kwa utaratibu tutakwenda kundi 'A' na 'B'. Kwa hivyo, katika karatasi ya kupiga kura kuna kundi 'A' ambalo lina wagombea wanaume sita kutoka CCM tuchague wawili. Halafu kundi 'B' lina wagombea watatu wanaume kutoka CUF tuchague mmoja. Tunaomba tugawe karatasi za kura kwanza.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe msisitizo tu kwamba ukifanya vyenginevyo isivyokuwa hivyo kura itakuwa imeharibika. Labda wakati huo huo niwape taarifa nimepeana mikono na Waheshimiwa Wajumbe wagombea wengi, lakini nataka nitoe taarifa kwamba kwa kawaida Spika hana kura. Sasa niwaombe wote wale walioniomba kwamba naomba radhi sana sitawapa kura maana sinayo. Hiyo ipo kwa mujibu wa katiba ibara ya 81 kwamba Spika yeye ana kura ya uamuzi tu pale ambapo kuna jambo lilioko mezani kura zimefungana, sasa yeye ataitumia kura yake ya uamuzi ili tupate kuendelea na shughuli hiyo na iwe imepata uamuzi. Kwa hiyo, naomba radhi sana kura yangu imekuwa haipo. Tuendelee kupiga kura. *(Kicheko/Makofi).*

Mkurugenzi wa Uchaguzi Katibu onesha sanduku lionekane kama hamna kura zilizotangulizwa.

**UTARATIBU**

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Spika, tunataka kujua idadi ya wapiga kura. Hilo ni jambo muhimu ili tujue wanaopiga kura wangapi na kura zetu zitakuwa ngapi.

**Mhe. Spika:** Mkurugenzi wa Uchaguzi tafadhali hesabuni wapiga kura.

**Katibu:** Mhe. Spika, tunahesabu idadi ya wajumbe wote waliokuwemo ndani ya ukumbi. Lakini pia hapa tungependa kusisitiza katika kundi la mwanzo unatakiwa uchague watu wawili, ukichagua watu watatu tayari kura imeharibika.

Kwa sababu katika kundi 'A' kuna wajumbe sita unatakiwa uchague wawili, ukichagua watatu au wanne kura hiyo itakuwa imeharibika.

**Mhe. Spika:** Kwa hiyo, idadi ya wapiga kura imeshajulikana?

**Katibu:** Mhe. Spika, bado wanahesabu.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tusubiri kidogo tunahesabiwa.

**Katibu:** Ni wajumbe 78.

**Mhe. Spika:** Wajumbe 78 wapo ukinitoa mimi ambaye sina kura. Kuna mikono sijui kama imeharibika au vipi.

**Katibu:** Naona mheshimiwa mwengine anaingia kwa hivyo tunarekebisha hesabu yetu itakuwa wapiga kura ni 79.

**Mhe. Spika:** Mkurugenzi wa Uchaguzi mfahamishe mpiga kura aliyeingia mwisho.

**Katibu:** Mheshimiwa, kuna kundi 'A' na kundi 'B'. Katika kundi 'A' kwenye karatasi ya kura kuna wagombea sita unatakiwa uchague wawili na katika kundi 'B' kuna wagombea watatu unatakiwa uchague mmoja.

**Mhe. Spika:** Kura ni siri. *(Kicheko)*

**Katibu:** Waheshimiwa tumemaliza uchaguzi wa makundi hayo mawili, kundi 'A' la wagombea wanaume kutoka CCM na kundi 'B' la wagombea wanaume kutoka CUF.

**Mhe. Spika:** Kabla ya kuendelea wacha nithibitishe Mkurugenzi wa Uchaguzi. Hivi kuna mpiga kura ambaye kura yake haijakusanywa, hakuna, endelea.

**Katibu:** Tunakwenda kwenye uchaguzi wa kundi 'C' na kundi 'D'. Kundi 'C' kuna wagombea watatu ambao hawa ni wanawake kutoka upande wa CCM tunataka tupate mgombea mmoja. Kundi 'D' kuna wagombea watatu wanawake kutoka CUF nako pia tunataka tupate mgombea mmoja. Kwa hivyo, tunaomba tugawe karatasi za kura.

**Mhe. Spika:** Kura zigaiwe.

**Katibu:** Sanduku liko tupu tunali-*lock* kabisa.

**Mhe. Spika:** Wajumbe mmethibitisha katika sanduku hamna kitu. Mkurugenzi waoneshe tena.

**Mjumbe fulani:** Hamna! *(Kicheko)*

**Mhe. Spika:** Nashukuru.

**Katibu:** Waheshimiwa Wajumbe nadhani kila mtu amepata karatasi ya kupigia kura au yupo aliyekuwa hajapata. Wote wamepata karatasi ya kupigia kura tukusanye kura.

**Mhe. Spika:** Nategemea kura zote zimeshakusanywa. Kuna Mhe. Mjumbe ambaye bado hajaweka kura yake kwenye sanduku, hakuna. Mkurugenzi wa Uchaguzi Katibu.

**Katibu:** Mhe. Spika, sasa tungeomba tupate mawakala wa wagombea kwa ajili ya zoezi la kuhesabu kura. Kwa hivyo, ni nafasi ya kila mheshimiwa ambaye yumo katika uchaguzi huu kuweka wakala wake kwenda kushuhudia zoezi la upigaji kura.

Tunaanza kundi la kwanza.

**Kundi (A) la Kwanza**

Mhe. Ali Abdalla Ali, wakala wako

**Mhe. Spika:** Kabla ya hapo, wakala ni sawa, lakini ruhusa pia mjumbe kwenda mwenyewe, au kanuni inasemaje?

Kwa hivyo, unaweka wakala au unaweza ukenda kushuhudia mwenyewe katika kazi hiyo ya kuhesabu kura. Pia wataje wale watu wa kwenda kuhesabu kura, ili waone na wajumbe wanaweza wakasema kama wanawaamini, watakwenda wenyewe au wanaweka wakala. Mkurugenzi endelea.

**Kundi (A) la Kwanza**

**Katibu:** Mhe. Ali Abdalla Ali, wakala wako.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Mhe. Ali Salum Haji wa Kwahani.

**Katibu:** Mhe. Hamza Hassan Juma.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba radhi. Nakubali kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma, ananiamini sana kama mnavyoniamini nyote, lakini kwa shughuli hii mimi nisingependa nikachaguliwa kuwa wakala wa mjumbe yeyote. Kwa hivyo, Mhe. Hamza Hassan nikuombe radhi sana, chagua mjumbe mwengine ambaye unaona anafaa, ambaye unamuamini kama unavyoniamini mimi.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Naamini meza.

**Mhe. Spika:** Anaamini meza. Kuamini meza maana yake ni kuwa wale wanaohesabu anawaamini.

**Katibu:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wakala wako.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Machano Othman Said.

**Katibu:** Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, wakala wako.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Salmin Awadh Salmin.

**Katibu:** Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando), wakala wako.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Nakwenda mwenyewe.*(Vicheko/Makofi).*

**Katibu:** Mjumbe wa mwisho katika kundi hili ni Mhe. Mussa Khamis Silima, wakala wako.

**Mhe. Mussa Khamis Silima:** Mhe. Mohammed Said Mohammed.

**Kundi (B) la Pili**

**Katibu:** Mhe. Asaa Othman Hamad, wakala wako.

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** Mhe. Hija Hassan Hija.

**Katibu:** Mhe. Haji Faki Shaali, wakala wako.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mimi naamini tume haiwezi kuchakachua, kwa hivyo tume naiwachia, yaani naamini meza.

**Katibu:** Mhe. Ismail Jussa Ladhu, wakala wako.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Naamini meza.

**Kundi (C) la Tatu**

**Katibu:** Mhe. Amina Iddi Mabrouk, wakala wako.
**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Nakwenda mwenyewe. *(Vicheko/Makofi).*

**Katibu:** Mhe. Shawana Bukheti Hassan, wakala wako.

**Mhe. Shawana Bukheti Hassan:** Mhe. Mohammed Aboud Mohammed.

**Katibu:** Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi, wakala wako.

**Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi:** Mhe. Ussi Jecha Simai wa Jimbo la Chaani.

**Kundi (D) la Mwisho**

**Katibu:** Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, wakala wako.

**Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak:** Naamini meza.

**Katibu:** Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, wakala wako.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Naamini meza.

**Katibu:** Mjumbe wa mwisho kundi hili ni Mhe. Zahra Ali Hamad, wakala wako.

**Mhe. Zahra Ali Hamad:** Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji.

**Katibu:** Mhe. Spika, sisi tuko tayari kwa ajili ya kwenda kufanya zoezi la kuhesabu kura. Kwa ruhusa yako tungekuomba uwahirishe kama kwa dakika thalathini (30) ili kwenda kuhesabu kura, tutakaporudi tuje na matokeo.

**Mhe. Spika:** Mkurugenzi hebu wataje watu wa kuhesabu kura ili wajulikane.

**Katibu:** Mawakala wenyewe walioteuliwa ni kama hawa wafuatao:

| **Mwakilishi** | **Wakala aliyemteuwa** |
|---|---|
| Mhe. Ali Abdalla Ali | Mhe. Ali Salum Haji. |
| Mhe. Hamza Hassan Juma | Anaamini meza. |
| Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Mhe. Machano Othman Said. |
| Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Mhe. Salmin Awadh Salmin. |
| Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Atakwenda mwenyewe. |
| Mhe. Mussa Khamis Silima | Mhe. Mohammed Said |
| Mohammed. | |
| Mhe. Asaa Othman Hamad | Mhe. Hija Hassan Hija. |
| Mhe. Haji Faki Shaali | Anaamini meza. |
| Mhe. Ismail Jussab Ladhu | Anaamini meza. |
| Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Atakwenda mwenyewe. |
| Mhe. Shawana Bukheti Hassam | Mhe. Mohammed Aboud |
| Mohammed. | |
| Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Mhe. Ussi Jecha Simai |
| Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Anaamini meza. |
| Mhe. Mwajuma Faki Mdachi | Anaamini meza. |
| Mhe. Zahra Ali Hamad | Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji. |

Tupo tayari kwa zoezi la kuhesabu kura. Maafisa ni Katibu wa Baraza la Wawakilishi akisaidiwa na Katibu Mezani. Kuna maafisa wengine watatu tayari tumekwisha kuwapanga tayari kwa shughuli hiyo watashiriki katika zoezi hilo nao ni:-

| | |
|---|---|
| Ndg Saleh Ali Saleh | Afisa Mdhamini Baraza la Wawakilishi Pemba |
| Ndg Salmin Amour Abdalla | Mkuu wa Divishen ya Sheria. |

| | |
|---|---|
| Ndg Amour Mohammed Amour | Kaimu Mkuu wa Divishen ya Utafiti. |

Kwa hivyo hawa watatu ndio watakaoshiriki na sisi katika zoezi la kuhesabu kura.

**Mhe. Spika:** Ilikuwa ni muhimu kuwajua maafisa kwa sababu wale walioamini meza maana yake wanawaamini hao.

Waheshimiwa Wajumbe, Katibu amekisia kwamba tuahirishe kiasi cha dakika 30. Lakini wacha ni seme tu kwamba kikao hiki sasa nakiahirisha kwa muda kiasi cha dakika 30. Basi tusiende mbali kwa sababu kuna uwezekano baadhi ya kura zikagongana na tukalazimika kwenye baadhi ya makundi tukarudia tena. Kwa hiyo tusitawanyike tukaondoka baada ya kiasi cha dakika 30 tuwemo ndani. Mara baada ya hapo nadhani matokeo yatakuwa yapo tayari, tutarudi tena ili tuweze kutoa matokeo na kuendelea na shughuli nyengine.

Kikao sasa nakiahirisha mpaka saa 4:00 asubuhi hii.

*(Saa 3:30 Baraza liliakhirishwa kwa muda wa dakika 70 mpaka 4:40 asubuhi)*

*(Saa 4:40 asubuhi Baraza lilirudia)*

## MATOKEO YA UCHAGUZI

**Mhe. Spika:** Kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuruni Waheshimiwa Wajumbe mmekuwa wastahamilivu kidogo, tulipanga tuchukue muda kama wa dakika 30, lakini hii kazi haikuwa ndogo na tumechukua muda wa saa nzima. Tunashukuru kwamba hakutakuwa na marejeo, mambo yamekwenda vizuri, mawakala wote wametia sahihi kukubaliana na matokeo haya.

Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe, nitoe matokeo ya upigaji wetu wa kura tulioufanya asubuhi, kuwachagua waheshimiwa watano wa Baraza hili ili watuwakilishe kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nao wabunge leo asubuhi walikuwa na kazi ya kumchagua Spika, baada ya hapo tunategemea watafanya kazi ya kuwaapisha Waheshimiwa Wabunge ambao tahari wapo Dodoma.

Wabunge watakaochaguliwa hapa tunategemea na wao Mungu akipenda wakajumuike na wenzao. Nimezungumza na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Kiongozi wa shughuli za Serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi hili atusaidie kuwachukua Waheshimiwa Wabunge hao kutoka Baraza ili wajumuike pamoja pale Dodoma *(Makofi).*

Kwa kuwa Mhe. Makamo wa Rais na yeye amepiga makofi inaelekea anakubali kuwachukua hao Waheshimiwa Wajumbe watakaokuwa wamechaguliwa na kutangazwa rasmi hapa.

Matangazo ya kura tayatolewa kwa mujibu wa makundi vile vile. Wataanza kutangazwa wale waliopata kura ndogo na kumalizia kwa aliyepata kura nyingi.

Waheshimiwa Wajumbe matokeo ya upigaji kura wetu tulioufanya hivi asubuhi ni kama ifuatavyo:-

Idadi ya wapigaji kura kwa makundi yote ilikuwa ni 79 ingawa mjumbe mmoja aliingia mwisho lakini na yeye aliwahi kupiga kura makundi yote.

**KUNDI (A)**

Jumla ya kura zilizopigwa na wajumbe wote wa Baraza la Wawakilini ni 79 na kura zilizoharibika ni 1.

| **Majina ya Wajumbe** | **Kura walizopata** |
|---|---|
| Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | 10 |
| Mhe. Ali Abdalla Ali | 14 |
| Mhe. Hamza Hassan Juma | 17 |
| Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | 22 |
| Mhe. Jaku Hashim Ayub | 42 |
| Mhe. Mussa Khamis Silima | 50 |

Kwa matokeo hayo naomba kuwatangaza rasmi Mhe. Mussa Khamis Silima na Mhe. Jaku Hashim Ayub kuwa wamechaguliwa na Baraza la Wawakilishi kuwa wabunge. (*Makofi*).

**KUNDI (B)**

Kura zote zilizopigwa ni 79, kura zilizoharibika ni 2.

| **Majina ya Wajumbe** | **Kura walizopata** |
|---|---|
| Mhe. Haji Faki Shaali | 8 |
| Mhe. Ismail Jussa Ladhu | 33 |
| Mhe. Asaa Othman Hamad | 36 |

Kwa matokeo hayo naomba kumtangaza rasmi Mhe. Asaa Othaman Hamad kuwa amechaguliwa na Baraza la Wawakilishi kuwa Mbunge (*Makofi*).

**KUNDI (C)**

Kura zote zilizopigwa ni 79, hakuna kura iliyoharibika na matokeo ni kama ifuatavyo:-

| **Majina ya Wajumbe** | **Kura walizopata** |
|---|---|
| Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | 13 |
| Mhe. Amina Iddi Mabrouk | 26 |
| Mhe. Shawana Bukheti Hassan | 40 |

Kwa matokeo hayo namtangaza rasmi Mhe. Shawana Bukheti Hassan kuwa amechaguliwa na Baraza la Wawakilishi kuwa mbunge. (*Makofi*).

**KUNDI (D)**

Kura zote zilizopigwa ni 79, hakuna kura iliyoharibika na matokeo ni kama ifuatavyo:-

| **Majina ya Wajumbe** | **Kura walizopata** |
|---|---|
| Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | 8 |
| Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | 24 |
| Mhe. Zahra Ali Hamadi | 47 |

Kwa matokeo hayo namtangaza rasmi Mhe. Zahra Ali Hamad kuwa amechaguliwa na Baraza la Wawakilishi kuwa mbunge. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye ni Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na maafisa waliomsaidia kufanya kazi hii. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kushiriki vizuri katika upigaji kura. Niwashukuru wale waliofanikiwa kuwa wabunge. Vile vile niwashukuru wale ambao hawakufanikiwa kuwa wabunge.

Baada ya shughuli hiyo Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa kazi nzuri mliofanya ili kuweza kufanikisha uchaguzi huu. Naomba wabunge wote waliochaguliwa wawasiliane na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ili kujua utaratibu wa safari ya kwenda Dodoma ambayo nafikiri sana itakuwa ni leo.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa tuendelee na shughuli iliyobakia.

**HOTUBA YA KUFUNGA BARAZA**

**HOTUBA YA MAKAMO WA PILI WA RAIS**
**MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI**

**ALIYOITOA WAKATI WA KUFUNGA MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR, TAREHE 12 NOVEMBA, 2010**

Mheshimiwa Spika,
Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana, Assalaama aleykum.

Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema, nguvu na uwezo wa kukutana kwa mara ya kwanza ndani ya Baraza lako hili tukufu kama wajumbe wa Baraza la Nane la Wawakilishi la Zanzibar. Tumekuwa pamoja takribani kwa muda wa wiki moja katika kutekeleza majukumu yetu. Naamini tumejifunza mengi katika kipindi hicho. Waliokuwa hawazifahamu sheria na kanuni za Baraza lako Tukufu sasa wanazielewa. Waliokuwa hawafahamiani sasa wanafahamiana.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wote wa Zanzibar kwa kupata fursa ya kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2010 na kuwachagua Wawakilishi, Wabunge na Madiwani katika majimbo mbali mbali ya Unguja na Pemba na kuiacha nchi yetu ikiwa bado imo katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Hii inadhihirisha wazi jinsi wananchi wetu walivyobobea katika kutumia demokrasia yao ya kuwachagua viongozi wawapendao kwa ridhaa zao kwa amani na utulivu.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza pia tena kwa dhati kabisa wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa kukipa ridhaa ya kuongoza kwa mara nyengine tena Chama Cha Mapinduzi kwa kukipatia ushindi mkubwa. Ni dhahiri imani ya wananchi juu ya Chama Cha Mapinduzi bado ni kubwa. Hii inatokana na Sera pamoja na Ilani nzuri za CCM katika kuwatumikia Watanzania.

Kwa heshima kubwa sana napenda kutumia nafasi hii tena kuwapongeza Marais wetu wawili, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kuchaguliwa kwa Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein kuwa Rais wa Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaonesha dhahiri imani kubwa waliyonayo wananchi wa Zanzibar juu yake na kwa Chama Cha Mapinduzi. Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ni mtu makini, mpole, mchapakazi, mwana demokrasia na msikivu. Sisi kama wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunamuahidi kushirikiana nae bega kwa bega katika kuiongoza nchi yetu ili kuleta maendeleo kwa watu wetu.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama nitasahau kukupongeza kwa dhati wewe Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine tena kuwa Spika wa Baraza hili tukufu. Kuchaguliwa kwako kumeonyesha imani ambayo waheshimiwa wawakilishi wanayo juu yako kwa vile umekuwa na uwezo mkubwa, uzoefu wako ni wa hali ya juu na umakini wako usiomithilika. Kwa kweli utendaji wako wa kazi ni wa kupigiwa mfano. Tunakuhakikishia ushirikiano wetu ili kwa pamoja tuweze kuwatumikia wananchi kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, pamoja na kazi ambayo Baraza hili imefanya ya kukuchagua wewe kuwa Spika, pia tulichagua wenzetu watano ambao wataliwakilisha Baraza kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ningependa kuwapongeza kwa dhati wajumbe hao watano wa Baraza lako tukufu waliochaguliwa leo hii kutuwakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa ruhusa yako naomba kuwatambua Wawakilishi wetu hao ambao ni :-

1. Mhe. Jaku Hashim Ayoub (CCM)
2. Mhe. Mussa Khamis Silima (CCM)
3. Mhe. Shawana Bukheti Hassan (CCM)
4. Mhe. Asaa Othman Hamad (CUF)
5. Mhe. Zahra Ali Hamad (CUF)

Ninawatakia Wawakilishi wetu kila la kheri na mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yao huko Bungeni. Pia ninawapongeza wale wenzetu ambao kura zao hazikutosha. Muda upo wa kujaribu tena hapo 2015.

Mhe. Spika, kama ulivyosema tutaongozana kesho kuanzia saa 1:00 asubuhi kwenda Bungeni ili tuweze kuapishwa pamoja.

Mhe. Spika, niruhusu pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wote wa Baraza hili kwa kuchaguliwa kuwa wajumbe wa Baraza la Nane la Wawakilishi. Wananchi wana imani kubwa na sisi hivyo tuna wajibu wa kuwatumikia ipasavyo hasa katika kusimamia maendeleo yao. Uongozi ni dhamana na sisi

kama wajumbe wa Baraza hili dhamana yetu kuu ni kuwatumikia wananchi wetu bila ya ubaguzi.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Namuahidi ushirikiano wangu wa dhati katika utekelezaji wa majukumu tuliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais kwa manufaa na maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika**,** baada ya pongezi hizo, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein kwa mamlaka aliyonayo kikatiba kwa kuniteuwa mimi kuwa Makamo wa Pili wa Rais, nafasi ambayo imenifanya pia kuwa kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza lako tukufu.

Naahidi kushirikiana kwa karibu sana na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu kwa kufuata sheria, kanuni na katiba ya nchi yetu ili tuweze kuwatumikia wananchi kwa ufanisi ambao ndio mategemeo yao. Katika kutekeleza jambo hili nitajitahidi kufuata matarajio ya watu wa Zanzibar ya kuwa na Serikali imara yenye kujali misingi ya kidemokrasia.

Mhe. Spika, katika suala zima la utulivu wa nchi yetu lazima tuwapongeze kwa dhati viongozi wa vyama vyetu walioasisi mtiririko mzima wa hatua hii ya amani tuliyofikia kuanzia katika vyama vyao, kamati zao hadi kufikia makubaliano kamili ambayo yametufikisha hapa tulipo sasa. Tumefanya uchaguzi wa aina yake mwaka huu na hata Jumuiya ya Kimataifa imetupongeza kwa namna tulivyoendesha uchaguzi wetu.

Mhe. Spika, baraza lako tukufu jana lilipata bahati adhimu ya kuzinduliwa pamoja na kuhutubiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein. Nachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa hotuba yake mahiri yenye maelekezo ya kina juu ya mipango na mikakati ya utekelezaji wa kazi za Serikali hii ya awamu ya saba chini ya Uongozi wake.

Mhe. Spika, sina haja ya kuirudia hotuba hio kwani sote tuliisikia hapa ukumbini na wengine katika vyombo mbali mbali vya habari. Sisi kama Waheshimiwa Wawakilishi tumeiunga mkono na kuiweka kama dira ya muelekeo wetu wa Baraza letu hili jipya la aina yake kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iwe dira kwetu. Hotuba hii imetusafishia na kutuonyesha njia ya wapi wananchi wa Zanzibar wanakotaka kwenda na namna gani

tutawafikisha huko. Tunataka kujenga Zanzibar mpya yenye mshikamano imara ambao siku zote utajali zaidi maslahi ya jamii yetu kuliko ya mtu mmoja mmoja, vikundi vya kijamii au vyama vyetu vya siasa.

Mhe. Spika, kwa kipindi kirefu tangu tuanze mchakato wa uchaguzi hadi sasa tumekuwa tukihubiri haja ya kujenga jamii yenye maelewano na mshikamano. Takriban kampeni za vyama vyetu vyote zilitawaliwa na wito wa kujenga Zanzibar mpya yenye mshikamano wa dhati. Wakati wa kipindi cha kampeni wengi wetu tulisikika majukwaani tukihubiri upendo na maelewano ya wananchi wa Zanzibar. Naamini ni kutokana na kauli zetu hizo ndio maana wananchi wetu wameamua kutuchagua. Hakuna wakati mwengine wa kutekeleza tuliyoyahubiri wakati wa kampeni zetu kama kipindi hiki cha baada ya kumalizika kwa uchaguzi wetu. Tuondoke hapa kurudi majimboni mwetu, tukiwa na lengo moja la kutekeleza kwa vitendo ahadi zetu za kujenga mshikamano, uelewano ambao tuliwaahidi wananchi wetu.

Mhe. Spika, amani na uchumi ni mambo yanayotegemeana. Mategemeo ya wananchi wengi baada ya uchaguzi Serikali yao itawasaidia kuimarisha maisha yao na kuwa bora zaidi. Serikali ya awamu ya saba imekusudia kujenga uchumi imara ambao utaondokana na utegemezi kwa kutambua wazi kuwa bila ya uchumi imara amani yetu tunayojivunia hivi sasa itakuwa mashakani. Kama tujuavyo njaa hujenga hasira ambazo hatimaye huzaa machafuko ndani ya jamii.

Katika kujenga uchumi imara jitihada zetu na wananchi wetu zinahitajika, kwani ‘mjenga nchi ni mwananchi na mbomowa nchi ni mwananchi pia’. Sote kwa pamoja tujitahidi kwa uwezo wetu wote kusimamia kazi iliyotukabili ya kujenga maisha bora kwa wananchi wetu, kwa kuongeza kasi ya uwajibikaji ndani ya majimbo yetu na ndani ya serikali.

Mhe. Spika, nidhamu na uwajibikaji wa kila mmoja wetu ni silaha muhimu ya kutufikisha tunakotaka kwenda. Tunahitaji nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali, tunahitaji nidhamu katika kukusanya mapato ya Serikali. Tunahitaji nidhamu katika matumizi ya mali za Serikali. Tunahitaji nidhamu katika kuendesha shughuli zetu za kila siku. Hotuba ya Mhe. Rais imesisitiza sana kuhusu jambo hili. Tulipokuwa tunamsikiliza akizungumzia jambo hili wengi wetu tulimshangilia. Naamini ushangiliaji wetu huu unaonyesha sote tunaunga mkono haja ya kuimarisha nidhamu na uwajibikaji katika kutekeleza shughuli za Serikali.

Mhe. Spika, Mhe. Rais pamoja na mambo mengine amezungumzia pia suala zima la elimu, utawala bora, kuimarisha muungano wetu. Kwa upande wa elimu Serikali ya awamu ya saba imekusudia kuimarisha elimu kwa njia mbali

mbali ikiwemo kujenga skuli mpya zenye vifaa vya kisasa kama vile vifaa vya maabara na kompyuta. Tunakotaka kwenda katika sekta ya elimu ni kuwa na elimu bora na sio bora elimu.

Mhe. Spika, nia ya Serikali ya awamu ya saba kama ilivyo awamu nyengine ni kuimarisha na kudumisha muungano wetu. Tutaendeleza na kuimarisha mahusiano ya Serikali zetu kwa lengo la kuondoa kwa kiwango kikubwa kero za muungano wetu. Tunaamini muungano imara ni faraja kwa kila mmoja wetu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha inapata haki zake stahiki katika muungano wetu.

Mhe. Spika, juzi tarehe 10/11/2010 nilipata bahati ya kushiriki katika warsha iliyoandaliwa kwa ajili ya Waheshimiwa Wawakilishi ili kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika vikao vya Baraza. Michango mingi ilitolewa katika warsha hio ambayo mengine ilihusu Serikali moja kwa moja.

Wajumbe wengi walizungumzia kuchelewa kupata miswada. Jambo hili linazorotesha utendaji wa wajumbe wako katika Baraza lako tukufu. Suala la wajumbe kupata miswada mapema ni haki yao ya msingi katika kutekeleza kazi zao. Suala hili nitalifanyia kazi kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili miswada iwafikie wajumbe mapema iwezekanavyo ili wapate muda wa kutosha kuisoma kwa kina.

Mhe. Spika, suala jengine lililojitokeza ni kuhusu majibu ya maandishi. Wajumbe wengi wamelalamika kuwa mawaziri wanapoahidi mbele ya Baraza lako tukufu kuwa watajibu baadhi ya maswali kwa maandishi huwa hawafanyi hivyo. Jambo hili ni kinyume na taratibu za Baraza lako tukufu. Waziri yeyote anapoahidi kujibu kwa maandishi anatakiwa kutekeleza ahadi hiyo. Nikiwa kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza lako tukufu nitalifuatilia suala hilo ili kila waziri anayeahidi kuwajibu Waheshimiwa Wajumbe kwa maandishi wafanye hivyo. Nitawasihi wale wenzetu watakaopata bahati ya kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa mawaziri ambao watatoka ndani ya ukumbi huu walizingatie jambo hilo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambao ni muhimu lililojitokeza katika warsha hio, ni kuwawezesha Waheshimiwa Wawakilishi kutembelea nchi za nje ili kuona wenzao huko wanafanya nini.

Ni jambo jema na nitalifuatilia suala hili kupitia kwa Afisi ya Mhe. Spika. Safari hizi zitatusaidia kuliimarisha Baraza letu na kulifanya liwe bora zaidi.

Mhe. Spika, Baraza letu ni Baraza la Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Nategemea katika kipindi chote cha miaka mitano tutafanya kazi bila ya mivutano au

malumbano yasiyokuwa ya lazima. Hii haina maana kuwa Serikali isihojiwe pale inapobidi, wajibu huu mkiwa wajumbe halali wa Baraza hili hautoondoka. Mategemeo yangu ni kwamba tutafanya kazi kwa nia moja ya kujenga Zanzibar mpya yenye maelewano ya kupigiwa mfano ndani na nje ya Tanzania.

Mhe. Spika, kabla ya kumalizia hotuba yangu hii, sina budi kukushukuru kwa mara nyengine tena kwa namna ulivyoliendesha Baraza hili tukufu kwa umahiri wa aina yake, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza kwa mashirkiano yao mazuri katika kusimamia shughuli za Baraza hili.

Mhe. Spika, sina budi pia kutumia fursa hii kuzishukuru nchi rafiki na mashirika mbali mbali ya kimataifa kama vile Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa yaani *UNDP* kwa misaada yao ya hali na mali na hasa katika kutusaidia katika kufanikisha uchaguzi mkuu wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii pia kuvishukuru vyombo vyote vya habari na wana habari wote kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kuwapatia habari wananchi wetu juu ya mambo mbali mbali ya maendeleo katika nchi yetu. Vile vile shukrani za dhati kwa watumishi na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri ya kuwahudumia Wajumbe wa Baraza hili muda wote. Ni matumaini yangu kwamba mashirikiano haya yataendelea kwa kiwango cha juu zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hotuba yangu hii, naomba sasa kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liakhirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 19 Januari, 2011 saa 3:00 asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Mhe. Makamo wa pili wa Rais tunakushukuru kwa hotuba iliyo safi ya kwanza kabisa katika Baraza hili na ni ya kwanza kwa Mhe. Makamo wa pili wa Rais kuitoa kwa Baraza letu la nane.

Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaamua hoja hiyo nataka niwakumbushe kwamba ile semina ambayo ilianza juzi itaendelea tena kesho pahala pale pale saa 3:00 asubuhi tunaombwa tuhudhurie semina hiyo ili tumalize ngwe ya kujielewesha mambo yanayohusu shughuli zetu za Baraza. Kwa hivyo, kesho kama kawaida semina itakuwa inaendelea saa 3:00 asubuhi pahala pale pale *Ocean View Hotel*.

Pili, mara baada ya shughuli zetu nataka nikumbushe tena kwamba kutakuwa na wimbo wa taifa kama vile tulivyoanza kwa kuufungua mkutano pale tarehe

09/11/2010 basi na kufunga mkutano tunamalizia kwa wimbo wa taifa letu la Zanzibar.

Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa tuliyoonesha katika shughuli zetu zote kwa kipindi hiki, namshukuru sana Katibu pamoja na watendaji wenzake kufanya kazi vizuri kwa mtiririko bila ya mapungufu yoyote. Niwaombe radhi Waheshimiwa Wajumbe kwamba juzi kwenye kikao chetu kulitokea mapungufu ya hapa na pale kutokana na matatizo ya umeme ni mambo ambayo tumeyaelewa tutajitahidi kushirikiana kwa karibu sana na serikali kuona kwamba tunapata *stand by generator* ili hali kama ile isitokezee, *generator* zilizopo hazitoshelezi kwa wingi wa umeme unaohitajika kutumika kwenye jengo hili, zipo mbili lakini bado hazitoshelezi. Kwa hivyo, serikali itafanya jitihada kuona kwamba tunapata *generator* nyengine inayofaa kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu kwenye jengo hili.

Waheshimiwa Wajumbe vile vile niwashukuru wale wote walioshirikiana na sisi katika kuendesha shughuli zetu hasa wenzetu wa habari, TVZ, redio pamoja na vyombo vyengine ambavyo vimesaidia tangu tulipoanza shughuli zetu katika ukumbi huu. Vile vile nawashukuru wageni wetu mbali mbali ambao wamekuja kuangalia shughuli zetu kwani wamekuwepo hapa kwa utulivu mkubwa na kwa heshima kubwa na imeongezea kunoga kwa shughuli zetu kwa wageni hao kuja kuangalia na kusikiliza yale yaliyokuwa yanaendelea katika ukumbi wetu huu.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa mliyoonesha katika kazi zetu. Kwa hivyo, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuliahirisha Baraza hili hadi tarehe 19/01/2011 saa 3:00 asubuhi wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 5:15 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano tarehe 19/01/2011 saa 3:00 asubuhi)*